JAMHURI YA KENYA
**WIZARA YA MAZINGIRA NA MISITU, MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA MISITU**
IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA
Dagoretti Corner, Ngong Road, P. O. Box 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya
Simu: 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4
Barua pepe: director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke
Twita @MeteoKenya

**Ref No: KMD/FCST/01-2024/SO/01(b)** **Issue Date: 29/02/2024**

## 1.1. TAARIFA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA KWA MSIMU WA MASIKA MACHI-MEI 2024

Kipindi cha mvua ya Machi-Mei ni kipindi cha mvua za masika katika sehemu nyingi nchini. Kiwango cha juu cha mvua (zaidi ya mm 300) hunakiliwa maeneo ya Ziwa Viktoria, Nyanda za juu za Magharibi, Katikati na Kusini mwa Bonde la Ufa. Vilevile Mashariki mwa Bonde la Ufa (pamoja na Nairobi) na mwambao wa Pwani.

Mvua nyingi inayozidi ile ya kawaida inatarajiwa maeneo ya Ziwa Viktoria, Nyanda za juu za Magharibi, katikati, kaskazini na kusini mwa Bonde la Ufa. Pia maeneo ya nyanda za Mashariki mwa Bonde la Ufa pamoja na maeneo ya Nairobi, Kaskazini Mashariki, Kusini Mashariki na Kaskazini Magharibi. Kwa ujumla, viwango vya mvua karibu ya wastani (average) na ya mwelekeo zaidi ya kawaida inatarajiwa kwenye maeneo ya Pwani na nyanda za chini za Kusini Mashariki. Dhoruba za mara kwa mara zaweza tokea wakati wa msimu.

Katika msimu huu, kuna uwezekano wa maeneo mengi kupata mgawo wa mvua wenye ujumla wa kuridhisha, isipokuwa kaskazini mashariki na kaskazini magharibi ambapo mgawo unatarajiwa kukaribia ule wa kiwango cha kuridhisha. Msimu unatarajiwa kuanza mapema ingawa kutakuwa na vipindi kavu mara kwa mara. Dhoruba za mara kwa mara zinawezatokea katika baadhi ya sehemu za nchi. Kilele cha mvua kinatarajiwa mwezi wa Aprili katika sehemu nyingi nchini isipokuwa sehemu za mwambao wa Pwani ambapo kilele kinatarajiwa kuwa mwezi wa Mei.

Hali ya joto nchini inatarajiwa kuwa zaidi ya wastani (average) katika maeneo yote ya nchi na yenye uwezekano mkubwa zaidi katika sehemu za pwani na Kaskazini mwa nchi.

### 1.1 Utabiri wa kina katika Msimu wa Masika (Machi-Mei) 2024 ni kama ifuatavyo:

#### 1.1.1 Ziwa Viktoria, Nyanda za juu za magharibi ya Bonde la Ufa na Kaunti za Katikati na Kusini ya Bonde la Ufa (Siaya, Kisumu, Homa Bay, Migori, Kisii, Nyamira, Uasin Gishu, West Pokot, Elgeyo Marakwet, Nandi, Kericho, Bungoma,

**Kakamega, Busia, Trans Nzoia, Vihiga, Laikipia (Laikipia West), Nakuru na Narok):**

Mvua inatarajiwa kuendelea kunyesha msimu mzima katika Kaunti hizi. Viwango vya mvua hii vinatarajiwa kuzidi vile vya kawaida. Mgao na muda wa kunyesha kwa mvua hii unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.

#### 1.1.2 Kaunti za Kaskazini Magharibi (Turkana na Samburu):

Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua za mara kwa mara katika msimu huu wa Masika. Viwango vya mvua hii vinatarajiwa kuzidi vile vya kawaida. Mgao na muda wa kunyesha kwa mvua hii unatarajiwa kuwa duni katika sehemu chache na wa wastani (average) katika sehemu zingine.

#### 1.1.3 Kaunti za nyanda za juu ya mashariki mwa Bonde la Ufa (Pamoja na maeneo ya Nairobi):

(Nyandarua, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka Nithi, na maeneo ya Mashariki mwa Laikipia): Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua nyingi wakati wa msimu huu wa masika. Mvua inatarajiwa kuzidi ile ya kiwango cha kawaida. Mgao na muda wa kunyesha kwa mvua hii unatarajiwa kuwa wa wastani na wa kuridhisha.

#### 1.1.4 Kaunti za nyanda za chini za Kusini-Mashariki ya Kenya (Kitui, Makueni, Machakos, Taita Taveta na Kajiado):

Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua nyingi katika msimu huu wa masika. Viwango vya mvua hii vinatarajiwa kuwa zaidi ya vile vya kawaida. Zaidi na hayo, Taita Taveta na sehemu za Kusini mwa Kaunti za Kitui na Makueni zinatarajiwa kupata mvua ya wastani na kuwa ingawa kuna uwezekano wa kupata kiwango kilicho juu ya wastani. Mgao wa mvua hii unatarajiwa kuwa wa wastani na wa kuridhisha.

#### 1.1.5 Kaunti za Kaskazini Mashariki (Mandera, Marsabit, Wajir, Garissa, Isiolo na baadhi ya maeneo ya Tana River):

Maeneo haya yanatarajiwa kupokea mvua ya mara kwa mara ikiwa na uwezekano wa viwango vyake kuzidi vile vya kawaida. Mgao na muda wake unatarajiwa kuwa duni katika sehemu chache na wa wastani katika sehemu zingine.

#### 1.1.6 Kaunti za Pwani (Mombasa, Tana River, Kilifi, Lamu na Kwale):

Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua kiasi kilicho karibu au zaidi ya wastani ikilinganishwa na msimu wa kawaida. Mgao na muda wa mvua hii unatarajiwa kuwa wa wastani na wa kuridhisha.

# 2 MATARAJIO YA TAREHE ZA MWANZO NA KIKOMO CHA MVUA ZA MASIKA 2024

## 2.1 USAMBAZAJI

Utabiri wa mwanzo, mwisho, na usambazaji wa mvua ya Masika 2024 umetayarishwa kwa njia ya kisayansi pamoja na uchambuzi wa takrimu za miaka iliyopita ambayo ilionyesha tabia nchi iliyo sawa na ya mwaka huu. Miaka inayofanana na mwaka huu ni 1998, 2010, na 2016. Vipindi vya kuanza kwa Msimu vinatarajiwa kuanza mapema hadi kawaida hasa katika maeneo ya Magharibi mwa nchi..

## 2.2 Tarehe za mwanzo na kikomo cha msimu

Tarehe za mwanzo na kikomo cha mvua za Masika katika Kaunti mbali mbali ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 1: Tarehe za Mwanzo na Kikomo**

| | Sehemu | Mwanzo | Kikomo | Hali ya Mgao wa Mvua |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Nyanda za juu Magharibi ya bonde la Ufa/Ziwa Viktoria, Katikati na Kusini mwa Bonde la Ufa ya Kenya** *(Bungoma, Trans Nzoia, Uasin Gishu, West Pokot, Elgeyo-Marakwet, Nandi, Kakamega, Vihiga, Bomet, Kericho, Kisii, Nyamira, Homa Bay, Migori, Kisumu, Busia, Baringo, Nakuru, Magaharibi mwa Laikipia na Narok)* | Mvua itaendelea kuanzia mwezi wa Pili | Huenda ikaendelea hadi Juni | Ya kuridhisha |
| 2 | **Kaunti zilizo nyanda za juu mashariki mwa Bonde la Ufa Pamoja na Nairobi** *(Nyandarua, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka Nithi, Nairobi na maeneo ya Mashariki mwa Laikipia)* | Mvua itaendelea kuanzia mwezi wa pili ila itafuatiwa na kipindi kikavu mpaka Machi, juma la tatu hadi la nne. | Kuanzia wiki ya nne ya mwezi wa Mei hadi ya kwanza ya mwezi wa Juni | Wastani hadi ya kuridhisha |
| 3 | Kaunti za nyanda za chini za Kusini Mashariki (*Kajiado, Kitui, Makueni, Machakos, Tana River na Taita Taveta),* | Mvua inatarajiwa kuanzia juma la kwanza la Machi ikifuatiwa na kipindi kikavu mpaka Machi, juma la tatu hadi la nne | Wiki ya pili hadi tatu ya Mei | Wastani hadi ya kuridhisha |
| 4 | Maeneo ya Kaskazini mwa Pwani (*Lamu, Malindi, mwambao wa pwani ya Tana River, na Kilifi)* | Mvua inatarajiwa kuanzia juma la nne la mwezi wa Machi, hadi juma la kwanza la mwezi wa Aprili | Huenda ikaendelea hadi juma la kwanza Juni | Wastani hadi ya kuridhisha |
| 5 | Maeneo ya Kusini mwa Pwani *(Mombasa, Kwale)* | Mvua inatarajiwa kuanzia juma la tatu hadi nne la mwezi wa Machi | Huenda ikaendelea hadi juma la kwanza Juni | Wastani hadi ya kuridhisha |
| 6 | Kaskazini Magharibi: (*Turkana, Samburu*) | Inatarajiwa kuanza kutoka juma la nne la | Wiki ya pili hadi | Duni hadi ya wastani |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Machi hadi juma la kwanza la Aprili (mvua ya mara kwa mara inatarajiwa kwa juma la kwanza la Aprili) | tatu ya Mei | |
| 7 | Kaskazini Mashariki (*Wajir, Isiolo, Garissa, Mandera and Marsabit*) | Inatarajiwa kuanza kutoka juma la nne la Machi hadi juma la kwanza la Aprili. | Wiki ya pili hadi tatu ya Mei | Duni hadi ya wastani |

## 3. ATHARI ZINAZOTARAJIWA KUTOKANA NA MVUA ZA MASIKA 2024

Mvua nyingi inayotarajiwa katika msimu huu wa Masika 2024 katika miezi ya Machi hadi Mei inatarajiwa kuleta athari mbaya hata kama itakuwa na manufaa katika sekta mbalimbali.

Habari Zaidi kuhusu athari kuu ambazo huenda zikatokea zitatolewa na wadau wa sekta husika.

***KUMBUKA: Miundo yote ya kimataifa ina ufanisi mdogo sana katika kutabiri msimu wa Machi hadi Mei kuliko msimu wa Oktoba hadi Disemba. Aidha, kuna mambo mengine yanayochangia mabadiliko kama vile vimbunga vya kitropiki na Mzunguko wa Madden Julian (MJO) ambayo yanaweza kutabiriwa kwa muda mfupi tu. Kwa hivyo, ni muhimu kusawazisha utabiri huu na utabiri mpya kila wakati.***


***Utabiri huu wa mvua za masika unatakiwa utumike pamoja na tabiri za hali ya hewa za siku 5, tabiri za wiki, tabiri za mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri na jumbe za athari pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti. Utapata habari hizi kwa Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini.***




Dr. David Gikungu

**MKURUGENZI WA IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA**


## Viambatisho





***Umbo 1: Machi-Aprili-Mei (MAM) "Mvua za Masika" Msimu (LTM)***





*Umbo 2: Machi-Aprili-Mei (MAM) 2024 "Msimu wa Masika" Utabiri wa Msimu*




*Umbo 3: Utabiri wa Hali ya Joto (MAM) 2024*




*Umbo 4: MAM 2024 Mwanzo wa Mvua*




*Umbo 5: MAM 2024 kikomo cha mvua*